**SHERIA YA KUANZISHA SHERIA YA MASUALA YA DIASPORA NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO**

---

## MPANGILIO WA VIFUNGU


**VIFUNGU** **MAELEZO**

**SEHEMU YA KWANZA**
**MASHARTI YA AWALI**

1. Jina fupi na kuanza kutumika.
2. Matumizi.
3. Ufafanuzi.

**SEHEMU YA PILI**
**MASHARTI YA KIUTAWALA**

4. Uteuzi wa mtu anaeshughulikia masuala ya Diaspora.
5. Kazi za Ofisi ya masuala ya Diaspora.

**SEHEMU YA TATU**
**HADHI NA FURSA YA DIASPORA KWA ZANZIBAR**

6. Diaspora.
7. Daftari la Diaspora.
8. Usajili wa Diaspora.
9. Uwezo wa Mtu aliyeteuliwa.
10. Taarifa.
11. Fursa kwa Diaspora waliosajiliwa.
12. Wajibu wa Diaspora.
13. Makatazo.

SEHEMU YA NNE
MASHARTI MENGINEYO


14. Jukwaa la Diaspora.

15. Kazi za Jukwaa la Diaspora.

16. Kongamano la Diaspora.

17. Makosa na adhabu.

18. Waziri kutunga Kanuni

SHERIA NAM. 4 YA 2020

NIMESAINI

{DKT. ALI MOHAMED SHEIN}
RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI
WA BARAZA LA MAPINDUZI

6 Mei ........................................................, 2020

# SHERIA YA KUANZISHA SHERIA YA MASUALA YA DIASPORA NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Masuala ya Diaspora, 2020 na itaanza kutumika baada ya Waziri kuitangaza katika Gazeti Rasmi.

Matumizi.

**2.** Sheria hii itatumika katika masuala yanayohusu Diaspora wote waliosajiliwa na wasiosajiliwa na kwa masuala yanayohusu Zanzibar.

Ufafanuzi.

**3.** Katika Sheria hii, isipokuwa kama maelezo yatahitaji vyenginevyo:

"Anao uhusiano na Zanzibar" maana yake ni mtu mwenye asili, uhusiano, mafungamano, kuasili au kwa kuungana na jamii ya Zanzibar kwa makubaliano ya pande zote mbili chini ya masharti yaliyokubaliwa;

"Mtu aliyeteuliwa" maana yake ni mtu aliyeteuliwa na Rais chini ya kifungu cha 4 cha Sheria hii;

"Jumuiya za Diaspora" maana yake ni Jumuiya zinazoundwa na Wanadiaspora aidha wakiwa ndani au nje ya Zanzibar;

"Jukwaa la Diaspora" maana yake ni chombo kilichoundwa chini ya kifungu cha 14 cha Sheria hii kinachofanya kazi maalum ya kushajihisha na kukuza mashirikiano ya Wanadiaspora;

"Diaspora" maana yake ni mtu aliyeelezwa chini ya kifungu cha 6 cha Sheria hii;

"Muda usio na ukomo" maana yake ni muda wa kuishi nchi za nje kwa Diaspora usiopungua miaka saba;

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya masuala yanayohusu Diaspora;

"Rais" maana yake ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

"Diaspora aliyesajiliwa" maana yake ni mtu aliyesajiliwa chini ya kifungu cha 8 cha Sheria hii.

## SEHEMU YA PILI
## MASHARTI YA KIUTAWALA

Uteuzi wa mtu anaeshughulikia masuala ya Diaspora.

**4.**-(1) Rais, kwa kupitia tangazo rasmi la Serikali, ataanzisha Ofisi na kumteua mtu ambaye atakuwa na dhamana ya kusimamia masuala ya Diaspora kwa Zanzibar.

(2) Mamlaka au cheo cha mtu aliyeteuliwa kitakuwa kwa mujibu wa amri ya Rais chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki.

Kazi za Ofisi ya masuala ya Diaspora.

**5.** Ofisi iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 4 cha Sheria hii itakuwa na kazi zifuatazo:

(a) kuwezesha upatikanaji wa fursa zinazotolewa chini ya Sheria hii;

(b) kuanzisha, kusajili na kutunza taarifa za Diaspora;

(c) kuwezesha masuala ya kifedha, hifadhi ya jamii, ardhi na masuala ya uwekezaji, biashara na masuala ya utalii;

(d) kuwezesha utoaji wa vitambulisho kwa mujibu wa Sheria Namba 3 ya 2018;

(e) kuwezesha upokeaji wa misaada na huduma za Diaspora;

(f) kushirikiana na Jumuiya za Diaspora na taasisi nyengine za kimataifa;

(g) kuhakikisha masuala ya Diaspora yanaingizwa katika sera na mipango ya kisekta;

(h) kushajihisha uanzishwaji wa Jumuiya mbali mbali za Diaspora;

(i) kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Sera ya Diaspora;

(j) kuimarisha mazingira yatakayowezesha Diaspora kujifunza na kukihifadhi Kiswahili na Utamaduni;

(k) kutoa fursa ya upatikanaji wa taarifa kwa Diaspora kupitia vyombo vya habari vya Serikali na tovuti rasmi;

(l) kuimarisha mahusiano ya kijamii na kiuchumi na Diaspora katika maeneo ya sayansi na maendeleo ya teknolojia mpya;

(m) kuandaa viwango vya utekelezaji vinavyopaswa kuzingatiwa na kufikiwa na Diaspora;

(n) kupanga na kutoa huduma za sekretarieti katika Jukwaa na Kongamano la Diaspora;

(o) kutoa uwelewa kwa jamii kuhusu masuala ya Diaspora; na

(p) kufanya mambo yoyote yanayohusiana na hayo.

## SEHEMU YA TATU
## HADHI NA FURSA YA DIASPORA KWA ZANZIBAR

Diaspora.

**6.**-(1) Kutakuwa na mtu atakayejulikana kuwa Diaspora ambaye amehama na kuishi nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa muda usio na ukomo wakati bado ana uhusiano wa undugu na Zanzibar.

(2) Mtu atatambulika kuwa ni Diaspora ikiwa atatimiza vigezo vifuatavyo:

(a) anao uhusiano na Zanzibar;

(b) anao utiifu kwa Zanzibar;

(c) anatambua na kuheshimu Mapinduzi ya Zanzibar ya 1964;

(d) anafuata Katiba na Sheria za Zanzibar na za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na

(e) anayo hati ya kusafiria ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au hati nyengine yoyote.

Daftari la Diaspora.

**7.**-(1) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 5 cha Sheria hii, kutakuwa na Daftari kwa ajili ya kutunza taarifa za Diaspora waliosajiliwa.

(2) Daftari litatunza taarifa za Diaspora zinazohusu:

(a) jina la Diaspora;

(b) utaifa;

(c) nchi anayoishi;

(d) jinsia;

(e) ujuzi na uzoefu; na

(f) taarifa nyengine zinayohusiana na masuala hayo.

(3) Taarifa na kumbukumbu binafsi zinazohifadhiwa katika Daftari zitakuwa ni siri.

Usajili wa Diaspora.

**8.**-(1) Diaspora anaweza kuomba kusajiliwa katika ofisi inayoshughulikia masuala ya Diaspora.

(2) Mtu aliyeteuliwa atalazimika kuchunguza maombi yaliyofanywa na Diaspora chini ya kifungu hiki kwa ajili ya kutathmini vigezo vya usajili.

Uwezo wa Mtu aliyeteuliwa.

**9.**-(1) Mtu aliyeteuliwa atakuwa na uwezo wa kukataa maombi ya usajili ya Diaspora ikiwa hakuridhika na vigezo vya usajili vilivyowekwa chini ya Sheria hii.

(2) Mtu aliyeteuliwa atakuwa na uwezo wa kufuta usajili wa Diaspora ikiwa yatakiukwa masharti ya Sheria hii.

Taarifa.

**10.**-(1) Mtu aliyeteuliwa atamuarifu kwa maandishi Diaspora sababu za kukataliwa maombi yake au kufutwa kwa usajili wake.

(2) Ikiwa Diaspora hakuridhika na maamuzi yaliyofanywa na Mtu aliyeteuliwa, anaweza kukata rufaa kwa Waziri ndani ya siku 30 kuanzia tarehe ya taarifa.

Fursa kwa Diaspora waliosajiliwa.

**11.**-(1) Kwa kuzingatia sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na sheria za Zanzibar, Diaspora aliyesajiliwa anaweza kunufaika na fursa zifuatazo:

(a) kusamehewa kibali cha kufanyia kazi;

(b) viza isiyo ya kikomo ya kuingia na viza ya muda mrefu ya kutembelea Zanzibar; na

(c) ruhusu ya kukaa muda mrefu ndani ya Zanzibar.

(2) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Diaspora aliyesajiliwa atalazimika kuomba fursa katika Ofisi inayoshughulikia masuala ya Diaspora.

Wajibu wa Diaspora.

**12.** Diaspora aliyesajiliwa atakuwa na wajibu wa:

(a) kutotumia vibaya fursa alizopewa kwa mujibu wa Sheria hii;

(b) kutangaza, kukuza na kulinda maslahi ya Zanzibar kuhusu utalii, uwekezaji, utamaduni, elimu, afya, michezo, sayansi na masuala ya misaada; na

(c) kudumisha na kuimarisha uhusiano baina ya Zanzibar na nchi anayoishi.

Makatazo.

**13.**-(1) Ni marufuku kwa Diaspora:

(a) kushiriki katika harakati za kisiasa ikijumuisha kujiunga na vyama vya siasa, kupiga na kupigiwa kura; na

(b) kuwa na haki nyengine yoyote ambayo ni mahsusi kwa Mzanzibari mkaazi kama Waziri atakapotangaza kila baada ya muda.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Diaspora aliyesajiliwa ambaye ni Raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ataendelea kupata haki zote kwa mujibu wa sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Zanzibar.

## SEHEMU YA NNE
## MASHARTI MENGINEYO

Jukwaa la Diaspora.

**14.**-(1) Kutakuwa na Jukwaa la Diaspora ambapo wajumbe wake watateuliwa na Waziri.

(2) Muundo wa Jukwaa la Diaspora utakuwa kama ulivyoelezwa katika Kanuni.

(3) Waziri atakuwa ni Mwenyekiti wa Jukwaa la Diaspora.

Kazi za Jukwaa la Diaspora.

**15.**-(1) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, Jukwaa la Diaspora litakuwa na kazi zifuatazo:

(a) kutoa ushauri kuhusu masuala ya Sera ya Diaspora;

(b) kuhakikisha uandaaji mzuri wa mikutano ya Diaspora;

(c) kushauri kuhusiana na utekelezaji wa Mkutano wa Diaspora;

(d) kupanga na kushajihisha mahusiano ya kiuchumi, utamaduni, elimu, afya, sayansi na michezo na Diaspora; na

(e) kushauri mazingira mazuri kwa mipango ya uwekezaji na miradi inayoanzishwa na Diaspora.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu hiki, Jukwaa la Diaspora linaweza kujiwekea taratibu zake.

Kongamano la Diaspora.

**16.**-(1) Kutakuwa na Kongamano la Diaspora litakaloendeshwa kama itakavyoonekana inafaa.

(2) Kongamano la Diaspora litahusisha Diaspora waliosajiliwa, wasiosajiliwa na wahusika wengine wa maendeleo kujadili masuala ya Diaspora na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Makosa na adhabu.

**17.**-(1) Itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote kuzitumia vibaya na kwenda kinyume na fursa zilizotolewa chini ya Sheria hii.

(2) Mtu atakayekwenda kinyume na masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, ametenda kosa na akitiwa hatiani, atapokonywa fursa zilizotolewa na atalipa faini isiyozidi Shilingi za Kitanzania Milioni Moja au kutumikia kifungo kwa muda usiozidi mwaka mmoja au vyote viwili kwa pamoja faini na kifungo.

(3) Mtu yeyote ambaye amemshawishi, amemshajihisha, ameshirikiana na Diaspora kufanya kosa, ametenda kosa na akitiwa hatiani, atalazimika kulipa faini isiyozidi Shilingi za Kitanzania Milioni Moja au kutumikia kifungo kisichopungua mwaka mmoja au vyote viwili kwa pamoja.

Waziri kutunga Kanuni.

**18.**-(1) Waziri anaweza kutunga Kanuni kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa masharti ya Sheria hii.

(2) Bila ya kuathiri uwezo wa jumla wa Waziri chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Waziri anaweza kutunga Kanuni mahsusi kuhusiana na mambo yafuatayo:

(a) kuweka muundo wa wajumbe wa Jukwaa la Diaspora;

(b) utaratibu wa kukata rufaa kwa Waziri; na

(c) kuweka vigezo na utaratibu wa usajili wa Diaspora ikijumuisha na gharama zilizoelezwa.

**UMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 1 Aprili, 2020.

..........................................

(RAYA ISSA MSELLEM)

***Katibu wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.***